# Galaxy express VBS

Pale ambapo watoto wanapata kukutana na ukuu wa Mungu!



# Mwongozo wa mkurugenzi

## Karibu kwenye ratiba ya 'galaxy express' VBS

Walimu wata furahi kubadilisha kanisa yenu ama eneo la klabu kuwa meli ya kwenda angani ambayo inajulikana kama the 'galaxy express' ambamo kila kikundi kita paa kwenda kwenye anga ya nje kuchunguza maajabu ya Mungu .Watoto watapata msukumo wa nguvu wanapokuwa waki peperuka ndani ya meli ya kwenda angani,wakiinama kutoka upande wa kushoto hadi upande wa kulia watakuwa wana fikiria kwamba meli inaenda upande iki epuka mawe makubwa ya anga .Nyimbo za kusikiza wakati wakupaa na kutua zitafanya fikira za watoto kupata uhai na pia michezo ya kuigiza wakiwa na nahodha na msaidizi wake 'roboti'.

Kila siku utapeleka watoto kwa safari kwenda kwa kituo anga,watoto wataweza kwenda kwa mwezi ama kwa sayari nyingine ama kwa nyota ambamo wata soma kuhusu ukuu wa mungu kutoka kwa maisha ya Musa.kila mtu atafurahi watakapo kuwa wana imba pamoja,wakimaliza na vitendo kwa ajili ya nyimbo.

Baada ya muda kwenye 'daraja'watoto wata tawanyika kwa madarasa ambayo yata husisha watoto wa umri mmoja na wata weza kuzunguka katika meli ya kwenda angani, pia wataelekea kwenye madarasa ya kadeti ambamo wanafunzi watafanyia kazi vitabu vyao na pia wapitie hilo somo,uhandisi nao watafanyia kazi ufundi na pia watafanyia kazi chumba cha maankuli kwa vitafunio na anga ombi kwa sababu ya somo.kwa hizi vikundi vidogo vidogo wanafunzi wako watapata kujuana vizuri na walimu wao, hapa wataunda urafiki mpya ambao utadumu mwaka mzima.

Ni rahisi kuita watoto nyuma pamoja kwenye 'daraja' kwa ajili yao kucheza michezo kadhaa ya anga.Funga siku kwa kuimba nyimbo kadhaa kutoka kwenye diski mpya 'galaxy express' na pia uongeze ombi, na usisahau kuwaalika tena wakuje kwenye VBS hio siku ambayo itafuata!

## Natarajia kuwa mta furahishwa Na hii likizo ya chuo cha bibilia . . . najua utaweka ubunifu mwingi Sana ndani yake Na kuifanya iwe 'nje ya hii dunia'



www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Utangulizi | 1 |
| Mikopo | 2 |
| Mtazamo wa juu | 3 |
| Jinsi ya kutumia hiki kifaa | 5 |
| Mawazo ya Ziada | 9 |
| Somo la 1 | 11 |
| Somo la 2 | 14 |
| Somo la 3 | 17 |
| Somo la 4 | 20 |
| Somo la 5 | 23 |
| Nyimbo | 26 |
| Raslimali za kutoa nakala | 30 |
| Ratiba kamili ya bure iliyoko kwenye tovuti | 33 |


## Watoto ni wa muhimu

www.ChildrenAreImportant.com


Nyenzo hii "Galaxy express"imeandikwa na wizara ya "watoto ni wa muhimu"na haki zote zime hifadhiwa.

Nyenzo yetu ni bure kutoa kwenye mtandao,bure kutumia, bure kupiga chapa na bure kusambaza kwa makanisa mengine na wizara bila majukumu



Kwa maelezo Zaidi,wasiliana na sisi:
info@ChildrenAreImportant.com or 01-52-592-924-9041


**asanti kwa siku mzima!**


Wahariri: Kristina Krauss

Creative Team of CAI: Dwight Krauss, Mike Kangas, Rubén Darío, Suki Kangas, Verónica Toj, and Vickie Kangas.



# Jopo la urambazaji

Maelezo ya Jumla

| | | |
|---|---|---|
| Itana kwake Mungu!<br>**Kuzaliwa kwa Musa**<br>Mungu ni Mkuu | Wakati wa somo hili, kila wakati wanafunzi wanaposikia "Mwite Mungu," ruhusu waitikie kwa kusema: "Bwana, Nisaidie!" Huku wakiruka na kuinua mikono yote miwili kuelekea kwa Mungu. | “Kwa sauti yangu namwita BWANA Naye aniitikia toka mlima wake mtakatifu.” Zaburi 3:4 |
| Itikia kwake Mungu<br>**Musa na Kichaka kilicho kuwa kina chomeka**<br>Mungu ni Waajabu | Wakati wa somo hili kila mara wanafunzi wanapo sikia haya maneno “Itikia kwa Mungu ‘wafanye wajibu kwa kusema “Ndio Bwana” huku wakiweka mikono yao kwa sikio. Kisha wanagongesha miguu yao pamoja kama askari huku wakisema “hapa nipo!”. | “Nimtume nani, naye ni nani atakaye kwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi” Isaya 6:8 |
| Tii Mungu<br>**Tauni zilizo kuwa misri**<br>Mungu ni Wakustaajabisha | Kila wakati wanafunzi wanaposikia "Mtii Mungu" wakati wa somo, ruhusu wanafunzi kujibu kwa kusema " Mimi lazima nisonge mbele " huku wakisimama na kubadilishana viti na wanafunzi wengine. | “Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa Huyo Roho aliyetupa.” Waraka wa kwanza wa Yohana 3:24 |
| Ngojea Mungu<br>**Wingu la kuwakinga na jua wakati wa mchana na nguzo la moto kuwapa joto wakati wa usiku**<br>Mungu ni Wakushangaza | Kila wakati wanafunzi wakisikia "Ngojea Mungu" wakati wa somo, wanafunzi wajibu kwa kusema "Niko tayari" huku wakiruka juu na kufanya ndondi, na kisha kusema "lakini mimi lazima nisubiri" wakiweka mikono yao pamoja na kukaa chini. | “Kwa maana Bwana ni Mungu wa hukumu; heri wote wamngojao.” Isaya 30:18 |
| Abudu Mungu<br>**Kuvuka bahari ya Shamu**<br>Mungu ni Wakutisha | Kila wakati wanafunzi wakisikia "Mwabudu Mungu" wakati wa somo, wanafunzi wajibu kwa kusema "Ninakuabudu" huku waki inua mikono yao juu katika anga na kukitikisa mbele na nyuma. | “Msifuni Mungu katika patakatifu pake; Msifuni katika anga la uweza wake.” Zaburi 150:1 |



www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili

| Chumba cha maamkuli | Darasa la Kadeti | Uhandisi | Michezo ya Anga |
|---|---|---|---|
| **Roboti**  Darubini |  | Musa katika kikapu  | Unda neno<br>Mtihani wa Ladha |
| **Kichaka cha musa kilicho kuwa kina chomeka**  Ukubwa wa kushangaza |  | Kile kichaka kilicho kuwa kina ungua  | Mbio ya Kunywa ya Relay<br>Mbio za kukula ndizi |
| **Mapigo**  Miondoko |  | Vua viatu vyako  | Mitindo za ajabu ya Sauti<br>Kichwa gamu |
| **Nguzo za Wingu**  Roketi za anga |  | Roketi ya Galaxy Express  | Kugusana juu ya mti kutengeneza piramidi |
| **Kuvuka Bahari katika Ardhi Kavu**  Supernovas |  | Kuvuka Bahari ya Shamu  | Kuangusha Marshmallow<br>Relay ya Keki |

# Jinsi ya kutumia kifaa hiki.

## VBS Ambayo ni Rahisi

Mkononi mwako umeshika VBS ambayo ni rahisi, rahisi kupanga na ni rahisi kutumia. Chukua tu tarehe, kusanya baadhi ya watu watakao jitolea, Weka baadhi ya mabango ya mwaliko katika maeneo yalio na jamii, na utakuwa tayari kwenda! Ukiwa na timu kubwa ya wafanyikazi, VBS ina raha zaidi kwa kila mtu ambaye atakaye husika, kwa hivyo tumeamua kugawanya hii kazi kwa vitengo kadhaa na majukumu ambayo yata husisha watu wengi.
Hapa tuna baadhi ya mawazo kwa ajili yako ili uweze kugawanya mzigo wa kazi wa VBS yako:

- Mkurugenzi 1 mkuu wa VBS.
- Kiongozi 1 wa Nyimbo.
- Mhubiri 1 wa somo kuu.
- Waigizaji 2 kwenye mchezo wa kuigiza (nahodha na roboti).
- Mratibu 1 wa darasa (vitabu vya wanafunzi na marudio ya somo).
- Mratibu 1 wa ufundi.
- Mratibu 1 wa vitafunio.
- Mratibu 1 wa michezo
- Viongozi 6-10 wa kila kundi ndogo, kulingana na idadi ya watoto kwenye VBS yako.

## Michezo ya kuigiza/ Michoro

Kila siku nahodha ataongoza watoto kwenye safari ndani ya meli ya anga "Galaxy Express" kwa usaidizi wa naibu wake roboti.
Nahodha wenu ni mtu wa kumaanisha sana kwani ana jukumu la kuongoza meli hii, pia ana jukumu la kuhakikisha kuwa watoto wamepata upokezo wa kiroho katika wiki hiyo. Anatambulisha msaidizi wake roboti kwa watazamaji: Anakaa machachari na saa zingine roboti huyu hafanyi kazi viruzi, Wakati mwingine roboti hunong'ona anapoongea, anaishia kunongo'na kutema nje sauti zisizo eleweka badala ya maneno. Kila wakati anahitaji mafuta kwenye viungo vyake ili aweze kuendelea kusonga.
Kila siku nahodha na roboti watawasilisha hoja kuu ya siku hiyo, na jinsi watoto wanavyo paswa kuitikia kila wakati wanapoisikia. Nahodha pia atawasilisha sehemu ya kutenda watoto watakayosikia katika vikundi vyao vidogo.
Mawazo ya michezo ya kuigiza yanatolewa kwenye ufunguzi wa kila siku, lakini pia unaweza funga siku nayo, au uwe na wahusika wakushiriki katika michezo au enda ukizunguka na utembelee madarasa. Watoto watapenda kupata kujuana na nahodha na roboti!

## Changamfu, katika Utendaji!

Kila siku, wanafunzi watajifunza usemi mmoja wa ile siku, na kuitikia kwa vitendo. Hii shughuli ni muhimu sana ili wanafunzi wako wasipate kuchoka wakati wa mahubiri makuu, na hii itafanya VBS yako yote maalum. Katika VBS mzima, wakati wowote kiongozi anataja usemi wa siku, wanafunzi wanafaa kuwa wanajua jinsi ya kuitikia na tendo linalo ambatana nao. Watajifunza wakati wa mchezo wa kuigiza na nahodha pamoja na roboti, na unaweza kutumia somo hili siku ile yote.

### Kupashana Ujumbe

Itana kwake Mungu!

Wakati wa somo hili, kila wakati wanafunzi wanaposikia "Mwite Mungu," ruhusu waitikie kwa kusema: "Bwana, Nisaidie!" Huku wakiruka na kuinua mikono yote miwili kuelekea kwa Mungu.

# Mpangilio

(21/2-Ratiba ya saa)

## Mwanzo wa nguvu!

Daraja

(Nyimbo-dakika 20
Mchezo wa wakuigiza wa ufunguzi-dakika 10)

## Dharula kutoka Udhibiti wa Misheni . . . .

(Somo kuu & Mstari wa kukariri-dakika 20)

….kwenye vituo

Chumba cha maamkuli

kituo cha vitafunio & utendaji katika anga.

Vituo vya Mzunguko - dakika 20

Uhandisi

(Kituo cha Ufundi)

Darasa la Kadeti

(Vitabu vya wanafunzi na kituo cha marudio)

…..kurudi kwa daraja….

## Michezo ya Angani

Daraja

(Michezo-dakika 30)

## Kadeti waondoke

(Wimbo wa kufunga & Matangazo-dakika 10)

## Vituo vya Mzunguko

Katikati mwa kila siku watoto watawanyika katika vikundi vitatu ambavyo watazunguka katika vituo hivyo: Ukumbi wa maamkuli ( kituo cha vitafunio na utendaji katika anga), uhandisi (ufundi) na darasa la kadeti (vitabu vya wanafunzi na marudio ya somo). Soma mengi kuhusu vituo kwenye ukurasa ufuatao.


## Michezo


Miechezo katika hii ratiba itachezwa na watoto wote wakiwa wameketi kwenye kikundi kikubwa na kugawanywa kwa timu kadhaa (unaweza kuwa na timu 2-4.) Kwa urahisi iwe ni kati ya wavulana dhidi ya wasichana. Kwa kila mchezo kila timu itatuma watu wachache ambao watajitolea kuwakilisha timu zao na wengine watakuwa wakisaidia wenzao ambao wanacheza kwa kupiga mayowe, kushangilia na kucheka kutoka kwa viti vyao. Ili watoto wasichoke kila wanapo cheza, wanafaa wachezeshwe michezo mbalimbali tofauti kila siku, kila mchezo utakua una chukua muda mfupi huku wakibadilisha wachezaji wengine wanaojitolea kushiriki kwenye mchezo. Wazo moja kwa ajili ya kuchagua wanafunzi ambao watashiriki kwanza katika mchezo , ni kwa kuangalia vizuri wanafunzi wenye tabia jema wakati wa shughuli zingine za VBS yako. Wape wanafunzi hawa kitu kitakachoonyesha kuwa watapata kushiriki kwenye michezo. Inaweza kuwa kitu kinachoninginia shingoni mwao, kitu kinachofungwa katika mkono wao au kadi ambayo wata iweka mfukoni mwao.Kwa kila mchezo, jinsi unavyo fanya matayarisho kabambe kabla ya wakati wa michezo, ndivyo michezo itakavyo kuwa ya kufana zaidi kwa wanafunzi wa VBS yako. Utakapokua unajitayarisha katika hii michezo, fikiria “michezo ya maonyesho ” au “ Nickelodeon” vipindi vya maonyesho katika runinga .Unaweza kua na vitambaa ambavyo vinang’aa na vitavaliwa na wanafunzi ambao watakuwa kwenye mstari wa mbele, na pia sauti athari au muziki wakati wa mchezo , na pia unaweza kuweka mapambo.(Tumepeana wimbo utakao chezwa wakati wa michezo ambao utachezwa kwenye CD ya Galaxy Express.) Mnaweza fanya vitu vya gharama ya chini ambavyo vitaongeza furaha katika VBS yenu. Kwa hivyo kueni tayari kuwa na raha na furaha!



www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili

# Vituo vya Mzunguko






## Chumba cha maamkuli


### Kituo cha vitafunio

Hapa utapata maagizo jinsi utakavyo tayarisha vitafunio. Weka kwa mawazo kua wanafunzi wanaweza furahia kwa kuunda vitafunio kama ufundi kabla ya kuvila. Usikose fursa ya kuwafunza wanafunzi wako jinsi ya kujifanyia usafi wenyewe baada ya kumaliza kupika vitafunio.

### Wazo

Utendaji katika anga kujadiliwa wakati wa kula vitafunio

Wakati wakula vitafunio, jadiliana na wanafunzi kuhusu utendaji katika anga na jinsi inavyo ambatana katika somo na maisha ya wanafunzi ya kila siku. Taarifa kuhusu vitafunio na utendaji katika anga zina patikana kwenye kijitabu cha kiongozi katika ukumbi wa maamkuli.









## Uhandisi

### Kituo cha ufundi

Hapa utapata wazo la ufundi, pamoja na mapendekezo na maelekezo ya vifaa hivyo. Vifaa vyote vya ufundi vinavyo patikana ndani ya Galaxy Express kwenye ratiba ya VBS vimebuniwa kutumia angalau karatasi moja kwa kila ufundi, hii inasaidia kwa kupunguza gharama iwezekanavyo. Kwenye tovuti una weza kutoa mifano, na pia utafute maelezo kuhusu ufundi kwenye mwongozo wa mkurugenzi na pia kwenye kijitabu cha viongozi wa uhandisi. Pia utapata mifano ya kutoa nakala kwenye kijitabu cha Uhandisi.

## Darasa la Kadeti

### Vitabu vya wanafunzi na kituo cha marudio.

Hapa utapata maelezo ya baadhi ya maneno muhimu kutoka kwa hadithi za bibilia katika lugha ya ishara. Rudia hadithi hio huku ukifunza kwa lugha ya ishara. Kisha peana vitabu vya wanafunzi na umsaidie yeyote ambaye ana maswali. Habari hii pia inaweza patikana kwenye kijitabu cha kiongozi wa darasa la kadeti.

**Familia**

Vidole gumba na kidole cha pili yakigusana, Fanya mzunguko wa nje hadi mikono igusane.





www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili



Huduma ya watoto mara mingi hua inapuuzwa,ina bajetiwa pesa kiasi ndogo na ina baadhi ya upuuzaji wa hali ya juu kwa huduma ya wakristo. Lakini kuna mamilioni ya watoto ambao wanahitaji kusikia kuhusu yesu!

**Ndio maana tuna weka muda wetu wote kutoa vya asili,vilivyo kamilika na shule la jumapili husika na mitaala ya chuo cha bibilia cha likizo,nyenzo za kufunzana,na raslimali kwa ajili ya Huduma ya watoto**

Tushaa unda nyenzo hizi kwa kihispania kwa ajili ya amerika kusini(latin America)

- *miaka 7 ya mtaala ya shule ya jumapili*
- *mitaala 7 ya VBS*
- *DVD 14 na maelezo ama densi kwa ajili ya ngoma*
- *CD'S 23 za muziki*
- *video na vijitabu vya kufunza*
- *kanda za filamu*
- *ratiba za pasaka na krimasi*
- *hila na vitabu za kupiga rangi*

Huu mwaka tuna enda India,kuanza na VBS na mitaala ya shule ya jumapili na raslimali ya kufunza walimu

Tunafanya hivi ju tunaamini kuwa

**Watoto ni wa muhimu**



www.ChildrenAreImportant.com

*Nyenzo yetu ni bure kutoa kwenye mtandao,bure kutumia, bure kupiga chapa na bure kusambaza kwa kwa makanisa mengine na wizara bila majukumu*

* Kama una nia ya kutuunga mkono kuandika nyenzo kwa lugha tofauti ,kutoa nyenzo zilizo pigwa chapa,ama kusambaza nyenzo zilizo pigwa chapa,tafadhali wasiliana nasisi. Tunaweza penda kuongea na wewe! *info@childrenareimportant.com*

# Mawazo ya Ziada

Uhandisi

## Ufundi wa ziada



Picha hii imeundwa na glue na kupakwa rangi ya unga au pambo. Inaweza kuwakilisha mlipuko wa furaha na sifa, kama ilivyo supanova! Ni furaha tunayo hisi wakati tunapo fikiri vile Mungu alivyo na yale ametenda kwa ajili yetu. Maelezo yanaweza sema, "Nitamwabudu Mungu."

Shughuli za ufundi: picha ya dunia kama inavyo onekana angani.



1. Chora duara kubwa katikati ya karatasi taulo kwa kutumia kalamu nyeusi au kalamu ya rangi isiyofutua na maji.
2. Wape  wanafunzi kalamu zilizo na rangi za kijani ili wapake  dunia rangi. Kisha  wapake maji na kalamu ya rangi ya (samawati) bluu.
3. Sasa ruhusu wanafunzi wapake na maji. Wanahitaji kutia duara nzima maji  na kutazama rangi ikichanganyika.
4. Mara inapo kauka, wanafunzi wakate kwenye mstari mweusi na kuweka glue ili washikanishe ubunifu wao kwa karatasi nyeusi.


## Shughuli  Darasani



Kila mtoto atengeneze wingu lake mwenyewe, na darasa liunganishe nguzo binafsi  la wingu la kila mmoja . Ili kuunda mawingu,  waruhusu waichore, kisha wakate , na kuweka pambo kwa glue. (Unga nyeupe  kutoka sokoni au pambo.) Rudia kwa safu ya miale ya moto.



Hapa kuna ufundi wa ziada wa kufurahisha unaweza kutumia! Kupamba fimbo upande mmoja kama moto na upande wa pili kama nguzo la wingu!




Mavazi hayo yatakuwa ya ajabu kwa walimu wako kutumia ili kuongeza ladha ya VBS yako! Funika lita 2 ya chupa za soda kwa karatasi ya nailoni au cellotape ya rangi ya kijivu, shikisha na karatasi ya tishu iwe miale ya moto kisha ufunge kamba ili ifungiwe kwenye mgongo wako. Walimu wako watapendeza wakiwa wamevaa " mifuko ya jeti" !

Watoto wata PENDA kuwa na picha kutoka VBS yako!





## Shughuli: Bonde la mwezi

Ruhusu wanafunzi wako kujenga mchanganyiko wa unga, na kisha angusha mawe madogo ndani yake. Tazama bonde zikitokea, mbele ya macho yako!
Mchanganyiko wa Unga: vikombe 4 vya unga na 1/2 kikombe cha mafuta





# 1 Safari ya kwanza


## Itana kwake Mungu!



Mabandari ya angani:
**Nebucopio**





### Mwanzo wa Nguvu

Mchezo wa kuigiza wa ufunguzi

Nahodha anakaribisha watoto kwenye wiki ilio jaa safari ya furaha wanapo safiri katika sayari kuona ukuu wa Mungu. Baadaye, anatambulisha msaidizi wake, Robot. Nahodha anaeleza jinsi leo wata watasafiri kuelekea Saturni na kutembelea kituo cha anga "Nebucopio" ambapo watakuwa wakitumia darubini za ajabu kuona sehemu za mbali sana. Nahodha pia anataja kwamba kila siku watakuwa wakijifunza kuhusu ukuu wa Mungu, moja kwa moja kutoka kwenye kitabu cha ajabu, cha kale sana, : Biblia. Tanguliza wimbo wa mwongozo nahodha akiwadhihaki watoto kwamba hawaonekani kuwa tayari kung'oa nanga safari ya mbali kuelekea angani, hivyo roboti anawasaidia kuwa tayari kwa wimbo. Ruhusu kiongozi wako wa wimbo kuongoza kila mmoja katika wimbo mkuu wa kung'oa nanga. Baada ya wimbo wa mwongozo, unaweza kutumia wimbo wa sauti ya athari kun"oa nanga na kusafari, ukiendelea na mchezo wa kuigiza katika safari.Meli ya kusafiri kwenye anga "Galaxy Express" inakutana na kundi la 'asteroids', na ina jaribu kuhepa ili isi gongane na moja. Roboti anapata hofu nyingi na anajaribu kupumua kwa nguvu kwa hofu ya ajali naye nahodha anamsaidia kujifunza kumwita Mungu.
Nahodha anafundisha watoto kuyasikiliza maneno ya siku, "Muite Mungu" na uitikie kwa usemi wa maneno, "Bwana, Nisaidie!" Huku watoto wakiruka juu na kuinua mikono yao kwa Mungu. Roboti anajaribu mara kadhaa na kujifunza maneno na vitendo pamoja na wanafunzi.
Mwishowe wako salama, na kufika Saturni. Roboti anadhani duara inayozunguka sayari ni barabara huru kwa ajili ya usafiri wa haraka. Wako na shida kutua, Hivyo Roboti anamlilia Mungu tena pamoja na watazamaji: "Mwite Mungu" na kila moja anajibu: "Bwana, Nisaidie"
Wao wanatua kwa wakati ili wapate mafunzo ya mwana anga kutoka katika Biblia! (Baada ya kutua salama kwa furaha na watazamaji, Anza somo kuu)



### Ujumbe unao ingia . . .

Mstari wa Bibilia

"Kwa sauti yangu namwita BWANA Naye aniitikia toka mlima wake mtakatifu." Zaburi 3:4




### Dharula kutoka kwa udhibiti wa Misheni . . .

Somo kuu

**Kuzaliwa kwa Musa**

Wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya ule utumwa, wakalia; kilio chao kikafika kwa Mungu kwa sababu ya ule utumwa. Mungu akasikia kuugua kwao, Mungu akakumbuka agano lake alilolifanya na Ibrahimu na Isaka na Yakobo. Mungu akawaona wana Israeli, na Mungu akawaangalia.
(Kutoka 2: 23-25) [Vyama vya biblia Kenya, Tanzania]

Biblia inatuonyesha katika Kutoka sura ya 2 kwamba watu wa Mungu walijifunza somo muhimu ambalo tunajifunza leo. Tunahitaji KUMWITA MUNGU tukiwa na hitaji la kitu chochote!




### Kupashana Ujumbe

**Itana kwake Mungu!**

Wakati wa somo hili, kila wakati wanafunzi wanaposikia "Mwite Mungu," ruhusu waitikie kwa kusema: "Bwana, Nisaidie!" Huku wakiruka na kuinua mikono zote mbili kuelekea kwa Mungu.



www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili




## Uchunguzi wa Angani


**Mungu ni Mkuuu**

Waisraeli walikuwa katika utumwa na walikuwa wakikabiliwa na matatizo katika maisha. Kuna wengi maskini, walio na chakula kidogo sana. Wakati mwingine tunahisi kudhihakiwa au kuchekwa shuleni au labda kuhangaika kwa sababu ya wazazi wetu wanaopigana wakati wote. Hapo ndipo tunahitaji KUITA MUNGU! Watu wa Mungu kwa wakati huu hawakuwa maskini tu na wenye njaa sana; lakini walikuwa walidhihakiwa pia na kuchekwa na Wamisri. Pamoja na matatizo yote, wangeweza pia kupigana miongoni mwao. Maisha yalikuwa magumu. Kisha kufanya mambo kua mabaya, mtawala wa Misri akatangaza kwamba watoto wote wakiume lazima wauawe! Hayo ni mateso makubwa !!! Kama mtu alihitajika KUMWITA MUNGU, ilikuwa ni Waisraeli.

Lakini Mungu alikuwa na mpango. Yeye kwa makini alitazama wakati Musa alizaliwa, na kumlinda asiuawe. Mamake Musa alijaribu kumficha kwa muda mrefu awezavyo asipatikane na wale askari wabaya wangemchukua na kumuua. Ukafika wakati hakuweza kumficha tena. Labda hiyo ni wakati alipata wazo nzuri sana: ya KUMUITA MUNGU! Mungu aka mchunga Musa huku mama yake akimuweka kwenye kikapu katika mtoni. Angeweza zama au kupelekwa mbali, lakini Mungu alihakikisha kwamba alikuwa salama. Kikapu kikaelea kuelekea karibu na nyumbani ya mtawala wa Misri ambapo bintiye farao aliamua kumchukua kama mtoto wake. Mungu wetu ni MKUU sana! Mungu alikuwa na mpango kwa maisha ya Musa na kumwona hata wakati alipokuwa mtoto katika kikapu, akielea katika mto. Mungu hukuona wewe na mimi na anajua kila mmoja wetu.

Tunaweza kujifunza somo muhimu leo KUMUITA MUNGU. Nyakati zaweza kuwa gumu kwako na kwangu. Kwa mfano, tunaweza kuwa na wakati mgumu shuleni au kupigana na ndugu. Jambo bora unaweza fanya ni KUMUITA MUNGU. Israeli walifanya hivyo. Waliweza KUMUITA MUNGU na Biblia inasema aliwasikia, na akawakumbuka. Mungu aliwaona na kuwajua. Akawa na huruma juu yao, na akawaokoa. Yeye alikuwa na mpango tayari kwa Musa ... mzaliwa Misraeli, na kuokolewa na mauti, alitoroka katika kikapu, na kulelewa katika familia ya Farao. Basi hebu tuweke katika matendo kile tulichojifunza leo na KUMUITA MUNGU!







## Chumba cha maamkuli

### Roboti

Kituo cha vitafunio

Anza na biskuti , chora roboti kuzunguka biskuti kwa karatasi, kisha weka peremende kwenye biskuti.
Au, tumia mafuta kidogo na mboga ilio katwa ili kuwa na robot mwenye afya. Unaweza pia kuanza na roboti ulio chora tayari kwenye karatasi ukipenda.





## Wazo

Utendaji katika anga kujadiliwa wakati wa kula vitafunio

### Darubini

Darubini ni vifaa vya ajabu. Tukiwa nazo tunaweza kuona upana mkubwa wa ulimwengu. Kutoka nchi, hatuwezi kuona sayari au mwezi vizuri kwa macho yetu. Wanaonekana kama maelfu ya alama ndogo angani. Lakini kwa darubini tunaweza kuwaziona kwa karibu zaidi. Tunaweza kuona mabonde katika sayari, anga na mambo mengine ya kuvutia. Kwa darubini, tunaweza kuona vitu vilivyo mbali vikiwa karibu.Wakati mwingine mimi na wewe huhisi kuwa wanyonge. Sisi ni kama mojawapo ya nyota ndogo katika ulimwengu ulio jaa nyota. Kuna wakati tunajihisi kama hakuna mtu anaweza kutuona sisi, lakini Mungu anaweza kutuona sisi kwa karibu. Ni kana kwamba ana darubini na anaweza kutuona sisi kwa karibu hata kama kuna maelfu ya watu wengine karibu nasi, na Anahisi kuwa umbali wa maili maelfu.



www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili

# Darasa la Kadeti



## Darasa la Kadeti

### Itana kwake Mungu!

Rudia hadithi, Ukifundisha maneno haya katika lugha ya ishara. Kisha peana vitabu vya wanafunzi na kusaidia yeyote aliye na maswali.

**Mtoto**

Mikono inayo pitana.



**Hofia / Ogopa**

Vidole vikigusana Fungua mikono funika kifua.



**Familia**

Vidole gumba na kidole cha pili vikigusana, Fanya mzunguko wa nje hadi mikono igusane.





# Uhandisi




## Uhandisi

### Musa katika kikapu

Yanayo hitajika:

Picha ilio tayari (Chapa, kata, na toboa mashimo)

Krayoni (au penseli za rangi, kalamu zarangi , au rangi)

Maelezo:

1. Wanafunzi waandike majina yao nyuma na kupaka rangi mbele.

2. Wanafunzi wapitishe kamba ndani ya mashimo.

# Daraja

## Kurudi hadi kwenye daraja kwa ajili ya michezo na kufunga

### Unda neno

Ukitumia watoto 3 kutoka kila timu, watoto watasimama kwenye jukwaa na kusema neno lenye herufi -3 watakao pewa wakitumia miili yao. Inaweza kuwa na awamu nyingi za kucheza, na kila timu itakuwa ikishindana dhidi ya nyingine katika mda uliowekwa. Wakati kiongozi anasema anzeni, kiongozi ananongonezea neno la kwanza kwa timu moja bila kuzungumza nao wanaunda neno kutumia miili yao. Watazamaji wa hiyo timu pekee watajaribu kubahatisha hilo neno. Wanapo kuwa sahihi, saa inasimamishwa kisha kiongozi ananakili sekunde ngapi ilichukua kwa timu yao kubahatisha neno sahihi.


Kama timu yako ni wavulana dhidi ya wasichana, wasichana watapata neno kwa mfano, na wasichana 3 walio kwenye jukwaa wata unda neno kwa miili yao wakati tu wasichana watazamaji wana pasa sauti kubahatisha neno hilo. Kama wavulana watahusika, wao watakuwa wanasaidia wasichana kushinda. Pendekezo la maneno yenye herufi 3 ni kama: Paa, Taa, Nzi, Tai, jua, Saa, Mto, Vua, nk.

### Mtihani wa Ladha


Karibisha jukwaani mtoto mmoja kutoka kila timu. Andaa vyakula tofauti vikiwa na ladha tofauti na miguzo tofauti. Ficha chakula kutoka kwa kila mtu, na funika macho ya wanafunzi wote wawili wanao kuja mbele. Leta chakula kimoja kwa wakati mmoja kwa wanafunzi walio jukwaani kisha ruhusu kila mmoja kuonja na kutambua ladha. Hakikisha Kuwa wanafunzi watazamaji watanyamaza kimya bila kutaja kile wanachokiona ili iwe changamoto kwa walio jukwaani. (Usiruhusu darasa lako kutoa majibu!) Kila mwanafunzi ana nafasi moja tu kutoa jibu, na wape sekunde 10 tu kuamua. Kuwa na kitambaa au taulo kupanguzia uchafu kama ikimwagika. Na wanafunzi jukwaani wawe na zamu ya kubahatisha aina ya vyakula tofauti. Timu ambayo inabainisha vyakula vingi zaidi inakuwa mshindi.


# 2 Safari ya pili

## Itikia kwake Mungu




Mabandari ya angani:
**Megantares**





### Mwanzo wa Nguvu

Mchezo wa kuigiza wa ufunguzi




Leo Roboti atakuwa na shida nyingi wakati wa kuwajibikia Nahodha, inaonekana ya kuwa amepoteza uwezo wa kusikia. Anza mchezo wa kuigiza nahodha akiwa anamsalimia 'Roboti', na pia akijaribu kuweka meli kuwa tayari kungoa nanga, lakini Roboti ana mpuuza kabisa. Huku wakingangana kuwasiliana, nahodha anafunza yule 'Roboti' na watazamaji jibu la siku hiyo.
Wakati wa somo hili, kila wakati wanafunzi wanapo sikia 'Itikia kwa Mungu' hakikisha kuwa wamejibu 'ndio  Bwana' huku wakiweka mikono yao kwenye sikio. Hatimaye na kugonganisha miguu pamoja kama askari huku wakisema 'hapa nipo' Nahodha anawaeleza kuwa watakuwa wanazuru 'Antares' leo,hii ni ile nyota ya kumi na tano kwa kuwa na mwangaza mwingi angani na ambayo pia ni  kubwa ajabu! Watatua kwenye kituo cha anga 'megantares' na kuona vile ulimwengu ulivyo mkubwa. (imba wimbo wa mandhari, kisha n'goa nanga kwa mlupiko wa wimbo wa sauti ya nguvu)Katika safari nahodha ana mtajia 'roboti' kuwa wanapaswa kushika njia ya nyota (nikama ni barabara huru) ili waweze kuwasili mwisho wa safari. Roboti hakusikia vizuri kwa hivyo wakakosa njia ya kuingililia kwenye njia ya nyota, na inabidi kuchukua nafasi inayo fuata. Nahodha ana weka 'oboti' mafuta na anaanza  kuitikia nahodha vizuri.(tumia msemo wa kukamata mara kadhaa: "Itika kwa Mungu" na "Ndio Mungu, niko hapa")
Wanatua wakati unao faa kwa kupata mafunzo ya falaki (astronauti) kutoka kwenye bibilia !
(Baada ya kutua kwa raha mkiwa na wasikilizaji, anza somo kuu)



### Ujumbe unao ingia . . .

Mstari wa Bibilia


"Nimtume nani, naye ni nani atakaye kwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi" Isaya 6:8



### Dharula kutoka kwa udhibiti wa Misheni . . .

Somo kuu **Musa na Kichaka kilicho kuwa kina chomeka**

Sasa musa alikua akichunga kundi la kondoo wake'Yethro' ,baba mkwe wake. Hapo ndipo malaika wa mungu alipojitokeza  kwa miale ya moto iliokuwa ikitoka kwenye kichaka. Musa aliona ingawa kichaka kilikuwa kina waka moto hakikua kina ungua ama kuisha. Kwa hivyo Musa akawaza, "nitaenda na kuona mtazamo huu wa ajabu- kwa nini kichaka hiki hakiungui"
Wakati Mungu alipoona kuwa ameenda kutazama, Mungu akamuita kutoka ndani ya kichaka, "Musa! musa!"
Naye Musa akasema, "niko hapa."
"Usije karibu tena," Mungu akasema. "Toa viatu vyako, kwa kuwa mahali unapo



### Kupashana Ujumbe

**Itikia kwake Mungu**

Wakati wa somo hili kila mara wanafunzi wanapo sikia haya maneno "Itikia kwa Mungu 'wafanye wajibu kwa kusema "Ndio Bwana" huku wakiweka mikono yao kwa sikio. Kisha wanagongesha miguu yao  pamoja kama askari huku wakisema "hapa nipo!".

simama ni mahali patakatifu." Kisha akasema, "Mimi ndie Mungu wa baba yako, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaaka na Mungu wa Yakobo." Kwa haya, Musa akaufícha uso wake, kwa maana aliogopa kumwangalia Mungu kwa macho yake.(Kutoka 3:1-6)
Ni ajabu jinsi Mungu wetu alivyo jionyesha na kuongea na Musa!!! Mungu alimwita Musa, na Alimjua kwa jina! Leo tunajifunza jinsi tunaweza kufanya Mungu anapotuita… ITIKIA MUNGU.

## Uchunguzi wa Angani

**Mungu ni Waajabu**


Musa alikuwa anaendelea na shughuli yake ya kawaida ya kuch unga kondoo wake baba mkwe wake. Musa hakuwa akiomba wala akifanya kitu chochote cha kiroho. Mungu alimuita alipo kuwa akifanya kazi. Yeye hakusema, 'Wewe hapo' bali Alimuita Musa kwa jina! Ghafla Musa alikuwa anasikia mtu akiita jina lake… "MUSA,MUSA." Lazima alikuwa akiangalia huku na huku akitafuta ni nani aliye kuwa akiita jina lake. Lakini hakukuwa na mtu karibu naye. Alikuwa pale peke yake. Kisha akaona. Kichaka kikiwaka moto!!! Unadhani alitoa kizima moto kwenye mkoba wake na kuanza kuzima moto uishe? Pengine aliharakisha kufanya kitendo ndipo alipo gundua kuwa kile kichaka haki kuwa kina ungua. Kilikuwa kina waka moto, lakini hakikuwa kina ungua! kisha kile kichaka kikaanza kuongea naye! Musa lazima angefikiria, " je naweza KUITIKIA MUNGU?"
Mimi na wewe kwa hali ya kawaida huwa hatuoni vichaka ambavyo vina chomeka, na pia Mungu huwa haongei na sisi kwa sauti ambayo tunaweza sikia, lakini Mungu anajaribu kuongea na sisi kila wakati. Mungu kila wakati hujaribu kuongea na wewe, kutumia muda na wewe ama kukupa mwelekeo. Hoja ni kuwa ni wachache wetu ambao huwa tunamsikiliza Mungu. Watu wengi huenda wakimpuuza Mungu siku nzima. Wao husahau kuwa Yeye Yuhai na anaishi na pia anataka kuongea na sisi! Mungu anatarajia kuwa UTAITIKIA KWA MUNGU!, JE MUNGU WETU SI NI MKUU?
Musa angeamua kupuuza Mungu kama vile tunavyo fanya leo, lakini alisimama na kusikiza. Kisha akafungua moyo na mdomo wake KUITIKIA alimjibu Mungu kwa usemi huu , "NDIO BWANA,NIKO HAPA." Mungu alikuwa na mpango wa kuokoa Waisraeli kutoka utumwani. Alitaka kutumia Musa. Musa aliitikia mwito wa Mungu wakati aliposema usemi huo rahisi, hakuna kikubwa , "Niko hapa". Mungu anataka kufanya mambo ya yaajabu katika maisha yako pia. Yuko na mipango mikuu kwa ajili yako, lakini anahitaji uache kile ambacho unafanya na umsikilize. Mungu anataka UITIKIE KWA MUNGU!

## Chumba cha maamkuli

### Kichaka cha musa kilicho kuwa kina chomeka

Kituo cha vitafunio

'Broccoli' inafanana kichaka kidogo cha rangi ya kijani kibichi na inawakilisha kichaka ambacho Musa aliona kikichomeka. Hata 'koliflawa'inaweza kulinganishwa na miti midogo. Tumbukiza kwenye (sosi) mchuzi wa nyanya ili ipate mfano wa moto. Ama mchuzi moto ili ipate hisia kweli ya moto.







## Wazo

Utendaji katika anga kujadiliwa wakati wa kula vitafunio

### Ukubwa wa kushangaza

Kwa kuwa Mungu ana jua majina yetu na anatupenda sana, tunaweza jihisi tukiwa wamuhimu sana na wakuu kwenye ulimwengu huu. Kama jinsi vile dunia inavyo onekana ikiwa kubwa ikilinganishwa na zuhura, mirihi, zebaki, na sayari kibeti.(onyesha bango la 2) lakini ukilinganisha dunia yetu na sayari zingine kubwa kama vile mshtarii, zohali,Uranus na neptun ,una hisi udogo wa dunia, (onyesha bango la 3) angalia mabango mengine ambayo yana onyesha ulimwengu huu. (onyesha bango la 4-6) kwenye upana mkubwa wa ulimwengu huu bado Mungu anaweza kukupata na anajua jina lako, lakini unahitajika kuitikia kwake anapokuita. Unaweza jihisi ukiwa wa maana sana, lakini katika ulimwengu mzima kwa kweli wewe ni mdogo sana sana sana sana.



www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili

# Uhandisi




## Uhandisi

### Kile kichaka kilicho kuwa kina uui

Vifaa vya kutumia:
Nakala ya picha Kwa kila mwanafunzi
Vipande vidogo vilivyo raruka vya tishiu
Penseli za rangi
Maelekezo
1. Tengeneza nakala za kichaka ama uwaache watoto waji choree kichaka.
2. Paka matawi rangi ya hudhurungi (maji ya kunde).
3. Kusanya pamoja karatasi za tishiu, zungusha karatasi kwenye kijiti ama penseli ya rangi ama kwa kalamu,kisha finyilia kwenye tone la glue kwenye picha ili uunde matawi na miale.
4.Watoto pia wanaweza chora vitu vingine kwenye picha zao kama vile mawe, korongo, jangwa, milima,jua, mawingu, n.k  Kama unao muda wacha wanafunzi wako wawe wabunifu.

# Darasa la Kadeti



## Darasa la Kadeti

### Itikia kwake Mungu

Rudia  hadithi, Ukifundisha maneno haya katika lugha ya ishara. Kisha peana vitabu vya wanafunzi na kusaidia yeyote aliye na maswali.

**Musa**



Panua kidole gumba na kidole cha pili kwa mikono yote  miwili kwa midundo: funga vidole vyako uki endesha mikono toka upande mmoja hadi mwingine.

**Malaika**



Miisho ya vidole kwenye mabega; vuta mbali na nje, ukipunga juu na chini.

**Skiza**



Funika sikio la kulia; geuza kichwa kuangalia upande wa kushoto

# Daraja

## Kurudi hadi kwenye daraja kwa ajili ya michezo na kufunga

### Mbio ya Kunywa ya Relay

Tumia watoto watatu kwa kila timu huku wakiunda foleni. Kwa upande mwingine wa chumba weka mtungi wenye maji juu ya meza kwa kila timu. Mpe mrija (straw) kila anaye shiriki  kwenye mchezo. Wanafunzi wata kimbia hadi kwa meza ambapo wataanza kunywa maji wakitumia mirija walio pewa hadi kiongozi apulize firimbi. Ata kimbia arundi na hapo mwenzake katika timu hio atakimbia na kuendelea kunywa maji. Timu ambayo itaibuka na ushindi ni ile ambayo itakuwa na maji kidogo ambayo yame baki kwenye mtungi baada ya muda ule ambao ulikuwa umewekwa kwa mchezo huokuisha.(ama kumaliza maji ndani ya mtungi)

### Mbio za kukula ndizi


Chagua mtoto mmoja kwa kila timu ambaye ata wakilisha wenzake kwenye mchezo huu, hapani kutoa maganda ya ndizi na kukula. Changamoto ambayo wachezaji watapata wakicheza huu mchezo nikua mkono moja unapaswa kuwa nyuma. Kiongozi akisema 'Enda', watoto wanapaswa kujaribu kutoa maganda ya ndizi kwa utaratibu kwa kutumia mkono mmoja na meno. Mara tu akimaliza kutoa maganda anakula ndizi na kumaliza ili awe mshindi kwa kumaliza akiwa wa kwanza.



www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili


# 3 Safari ya tatu


## Tii Mungu




Mabandari ya angani:

**Velocistar**








## Mwanzo wa Nguvu

Mchezo wa kuigiza wa ufunguzi


Leo Robot analalamika kwa sababu hakupata usingizi wa kutosha usiku uliopita, na anataka kulala kidogo. Kila wakati nahodha akimwomba kuandaa kitu ili waondoke, robot hataki kutii, na pia anaonekana kuchoka. Wanapo pambana sababu robot hataki kusikia, fundisha watazamaji neno la siku: 'Mtii Mungu' na majibu. Watazamaji wanajifunza kwa kuruka juu na kuanza kuandamana na kusema "Mimi lazima nisonge mbele," kisha badili viti na mtu mwingine! Wazo la somo la leo ni kwamba watazamaji daima wanabadilisha viti, kuwaweka tayari na kusikiliza maneno: ". Mtii Mungu"
Robot hafanyi hivyo vizuri mwanzoni na kurusha kelele zaidi kuliko kuzungumza, lakini nahodha anampa robot Coca-cola kubwa ulio na caffeine nyingi ili kumwamsha. (Tengeneza coke kubwa kujifanya au kahawa kutoka ubao au kadi)
Sasa robot anatembea kila mahali, kwa kasi zaidi kuliko roketi ya anga, au nyota, au kasi ya mwanga!
Imba wimbo wa kufungua, na kuondoka kuelekea anga. Wakati huu robot anatambua kuwa hajui wapi wanakokwenda, hivyo nahodha anamueleza. Wataelekea kwenda kwa nyota ya karibu na kutua katika kituo cha anga "Velocistar" ambapo watakuwa wanajifunza kuhusu mwendo. (Wakati wote robot anatembea kila mahali.)
Ruhusu kutua haraka ili safari hii iwe safari fupi ya wiki nzima (kwa sababu tunatembelea nyota ilio karibu sana), kisha muingie ndani ya somo. Robot anaweza kimbia kimbia kama kichaa wanapotua, huku nahodha akimkimbiza mara tu baada ya kutoka nje.



## Ujumbe unao ingia . . .

Mstari wa Bibilia

"Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa Huyo Roho aliyetupa." Waraka wa kwanza wa Yohana 3:24




## Dharula kutoka kwa udhibiti wa Misheni . . .

Somo kuu

Tauni zilizo kuwa misri

"Na sasa kilio cha wana wa Israeli umenifikia, na nimeona jinsi wanavyo kandamiswa na Wamisri. Hivyo sasa, nenda. Nakutuma kwa Farao ili upate kuwatoa watu wangu Israeli kutoka Misri ... sasa nenda; Mimi nitakusaidia kuongea na kukufundisha kile utasema. "Lakini Musa akasema," Msamehe mtumishi wako, Bwana. Tafadhali tuma mtu mwingine. "Kisha hasira ya Bwana ikawaka juu ya Musa ...
Kisha Musa akarudi kwa Yethro baba mkwe wake na kumwambia, Nataka kurudi Misri kwa watu wangu wenyewe ili kuona kama bado wako hai."
(Kutoka 3 : 9-10, 4: 12- 18)"



## Kupashana Ujumbe

Tii Mungu

Kila wakati wanafunzi wanaposikia "Mtii Mungu" wakati wa somo, ruhusu wanafunzi kujibu kwa kusema " Mimi lazima nisonge mbele " huku wakisimama na kubadilishana viti na wanafunzi wengine.



www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili

Kutii ni jambo gumu sana. Hakuna anayetaka kutii. Hakuna anayetaka kuacha kile anachokifanya na kutii mtu mwingine. Inaweza kuwa rahisi kukosa KUMTII MUNGU sababu hatumuoni, na hivyo tunajifanya yeye haipo ili tusiweze kumtii. Kila mtu anataka kufanya jambo lake mwenyewe. Kama hutaki kutii wazazi wako, ujuwe nini, wewe hauko peke yako! Binadamu wote walizaliwa hivyo. Sisi sii viumbe vidogo tu kama unavyo fikiria. Tulizaliwa na ubinafsi, tukifikiri kuwa dunia nzima inatuhusu sisi tu. Wakati mwingine tunapopaswa KUTII MUNGU na hatutaki, tunaanza kulalamika na kuomba kuondoka hapo. Naam, hivyo ndivyo Musa alifanya. Mungu alikuwa na mpango wa ajabu ili kuokoa watu wake kutoka katika utumwa na ukandamizaji. Alitaka kuonyesha utukufu wake na ukuu wakati huo huo anapokomboa watu wake. Akaamua kutumia mapigo, mfululizo wa mambo mabaya, kila mmoja ikizidi kuwa mbaya hadi Wamisri walipo ruhusu watu wake kwenda, na basi Mungu kuwa mshindi. Mungu alitaka Musa kuwa ndiye atakaye zungumza na Farao. Musa alikuwa jamaa wa Mungu, lakini Musa hakutaka kutii. Musa hakutaka kwenda. Musa akamsihi sana, akisema kwamba yeye si msemaji nzuri wa umma, na kwamba ni bora Mungu kutafuta jamaa mwingine. Musa akaomba Mungu kutuma mtu mwingine !!! Je, umewahi omba mama yako ili usiende mahali fulani au kufanya kitu? Basi, unajua jinsi Musa alihisi. Mungu alikuwa na mpango kubwa, na ilikuwa muhimu kwa Musa KUMTII MUNGU. Mungu akachoka na malalamiko Musa alikuwa akifanya. Biblia inasema kwamba Mungu akawa na hasira juu yake! Mungu akaruhusu Musa kupatana msaada, jamaa mwingine kwenda pamoja naye. Je, unafikiri Musa alifanya nini ??? Hiyo ni sawa, mwishowe ali MTII MUNGU!

Mpango wa Mungu ulionyesha utukufu wake na ajabu kwanza kwa kufanya fimbo ya Musa kuwa nyoka na kisha kurejea kuwa fimbo. Farao akakataa kuruhusu watu wa Mungu waende, kisha Mungu akaanza na mapigo, kila wakati akimpa Farao nafasi ya kutubu, lakini hakutaka. Kisha Mungu akatuma pigo baada ya pigo: damu, vyura, chawa, nzi, kifo cha mifugo, majipu, mvua ya mawe, nzige, giza, na kifo cha mzaliwa wa kwanza. Baada ya yote hayo, Farao hatimaye akakubali na basi Mungu akawa mshindi! Watu wa Mungu walikuwa huru kuondoka. Na wameona utukufu wa Mungu!

Yote yaliyotokea kwa sababu Musa alikuwa tayari kuacha kulalamika, kuondoka na kwenda, na KUMTII MUNGU!


## Uchunguzi wa Angani

Mungu ni Wakustaajabisha

## Ukumbi wa Maamkuli

### Mapigo

Kituo cha vitafunio






## Chumba cha maamkuli

Onyesha wanafunzi jinsi ya kukusanya chura kutoka viungo mbalimbali. Tumia tunda la tufaha ndogo au cookie kama mwili. Zabibu kijani, celery, au pretzels kuwa miguu. Macho ni pipi, raisons, au vipande vya chocolate juu ya marshmallows ndogo. Ulimi ni kiasi kidogo cha karoti. Waache watoto watengeneze vyura vyao wenyewe kwa ajili ya kujifurahisha.

Hiari: Ili kutoa maji mwekundu uliogeuka kuwa damu, weka mapema mchanganyiko mwekundu wa unga wa kinywaji chini ya chombo cheusi. Mwagia maji safi kutoka kwa glasi huku wanafunzi wakiangalia. Unapo koroga, itakuwa nyekundu.



**Wazo** Utendaji katika anga kujadiliwa wakati wa kula vitafunio


### Miondoko

Mungu aliyeteua muondoko katika ulimwengu. Alipanga tangu mwanzo kwamba dunia itakuwa inazunguka kwenye njia vile inavyozunguka jua. Lakini kutoka ardhini, hatuhisi kama tunasonga hata! (ruhusu watoto wazunguke duara kisha wajaribu kutembea upande wa pili wa darasa wakizunguka) Je, si ni vigumu kutembea kama tunaweza kuhisi ardhi ikipinduka na kuzunguka? Kama vile Mungu alipanga muondoko katika ulimwengu, Alipanga pia miondoko katika maisha yetu. Mpango wa Mungu kwa maisha ni pamoja na hatua ya kuchukua, kujihatarisha, na kumtii hata wakati njia ina onekana vigumu au mwendo kama kichaa. Kwa kweli, bila muondoko, sisi huchoka haraka na kuanza kutafuta mambo mengine ya kutufurahisha. Kama vile nchi inavyozunguka, Mungu ataendelea kutupa mwelekeo katika maisha yetu. Mwitikio wetu unahitaji kuwa, "Ndiyo Bwana" na muondoko.



www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili








## Darasa la Kadeti

# Itana kwake Mungu!

Rudia hadithi, Ukifundisha maneno haya katika lugha ya ishara. Kisha peana vitabu vya wanafunzi na kusaidia yeyote aliye na maswali.

### Hifadhi



Fungua mikono uliopinda.

### Mungu




Elekeza kidole ; Teremsha kisha fungua mkono katika kifua.

### Pamoja




Gusa ngumi pamoja.

### Enenda




Mkono wa kulia uelekee mbele ukifunga .







## Uhandisi



# Vua viatu vyako




vifaa:
Karatasi , Uzi au kamba, mbili kwa kila mwanafunzi , chombo cha kutoboa, Makasi, kalamu , kalamu ya alama.

maelezo:

1. Chora mguu wa mtoto ( watoto wanaweza kutumia miguu ya kila mmoja kuchorea. ) Kwenye karatasi au povu .
2. Kata sura ya kiatu , toboa mashimo ya kuweka kamba .
3. Patia kila mtoto vipande viwili vya uzi ili kufungia viatu miguu zao.


Msiwe na wasiwasi ya kufanya kuwa kamilifu. Watoto wadogo hupenda kufunga kamba na inawafundisha misuli ndogo uratibu. Watoto wakubwa hufurahia kutumia kamba ndefu na kufunga viatu vyao vizuri.

4. Andika yafuatayo juu ya viatu : Nitamjibu Mungu, "Ndiyo Bwana, Mimi hapa. "



## Kurudi hadi kwenye daraja kwa ajili ya michezo na kufunga

# Mitindo za ajabu ya Sauti




Kiongozi kuandaa kabla ya wakati orodha ya mitindo za sauti:
1. Kukohoa. 2. kwikwi. 3. Burp. 4. Chafya. 5. kupiga makofi. 6. Kupiga bisi 7. Kucheka. 8. Kugonga chini na miguu. 9. Kutengeneza koo.

Panga kwa mistari wachezaji sita, 3 kutoka kila timu, ukiwabadilisha . Eleza wachezaji kwamba ni lazima wafanye sauti zote wewe unafanya na kufuata mpangilio wako. Fanya sauti ya kwanza kwenye orodha. Teremka chini huku wachezaji wote wakitoa sauti kila mmoja. Kisha fanya sauti ya kwanza na ya pili, na wachezaji wote lazima watoe hizo sauti pia. Kisha ongeza sauti ya tatu, na kadhalika. Kama mchezaji hawezi fanya sauti, sahau sauti, au kufanya makosa mpangilio; Huyo mchezaji anaondolewa. Endelea kuongeza sauti mpaka mchezaji mmoja tu anabaki. Timu yake inakuwa mshindi!




**Kichwa gamu** Funga mkanda wa gamu (gamu upande wa nje) kwa paji la uso na eneo la kidevu, mtu mmoja kwa kila timu. Tawanya vipande vya karatasi katika meza. Wachezaji waweka mikono yao nyuma yao huku wamesimama nyuma ya meza, wakitazama watazamaji. Unaposema, "Nenda" Wachezaji wanabiringisha vichwa vyao katika meza, na kujaribu kukamata vipande vya karatasi vingi iwezekanavyo kwa vichwa. Mchezaji wa vipande zaidi dakika inapokwisha anakuwa mshindi.
(Mtoto akiwa na nywele ndefu vuta nyuma kabla ya kuweka mkanda ili kuepuka maumivu ya kuvutwa nywele)


# 4 Safari ya nne

## Ngojea Mungu

Mabandari ya angani:


**Panasa**





### Mwanzo wa Nguvu

Mchezo wa kuigiza wa ufunguzi




Fungua VBS ya leo nahodha na robot wakipigana kujadiliana sehemu watakao safiri. Nahodha anasema wanahitaji kwenda kwa mwezi, lakini robot anataka kwenda katika kituo cha satellite. Wanapambana huku na kule wakijiandaa kuondoka. Endelea na nyimbo katika-kati ya mapambano ili kuonekana refu. (Imba wimbo, na kisha wao wakimbie katika jukwaa, kisha imba wimbo mwingine, nk)

Ruhusu nahodha kufundisha robot somo la leo na majibu: Kiongozi anaposema "Ngojea Mungu", watoto waruke na kufanya ndondi huku wakisema "Niko tayari," kisha kuweka mikono yao pamoja na kukaa chini wakisema, "Lakini mimi lazima nisubiri."

Robot anatambua kwamba yeye alikosea na kuomba nahodha msamaha. Nahodha anakubali kwamba satellite ni wazo nzuri pia, na kusema wanaweza kwenda huko kesho ikiwa robot anataka, sababu mwanaanga tayari anasubiri katika mwezi kwa somo la leo. Nahodha na robot wanafuraha kupata suluhisho, mwezi leo na kesho ni satellite, hivyo wanakumbatiana na kujiandaa kwa ajili ya kuelekea mwezi. Kabla ya kuondoka, robot anaanza kutafuta viatu vyake vya buti za kwenda mwezi.


Nahodha anaeleza jinsi watakuwa wakitua katika "Kituo cha Panasa" na watakuwa wakijifunza kuhusu meli za anga na kusubiri. (Tengeneza safari haraka na kutua juu ya mwezi kwa somo.)



### Ujumbe unao ingia . . .

Mstari wa Bibilia

"Kwa maana Bwana ni Mungu wa hukumu; heri wote wamngojao."
Isaya 30:18




### Dharula kutoka kwa udhibiti wa Misheni . . .

Somo kuu **Wingu la kuwakinga na jua wakati wa mchana na nguzo la moto kuwapa joto wakati wa usiku**

Farao anapokaribia, wana wa Israeli walitazama juu, na Wamisri walikuwa wakiwafuata. Walipata hofu na kumlilia Bwana. Wakamwambia Musa, "Ilikuwa ni kwa sababu hapakuwa na makaburi katika Misri kutuleta jangwani kufa? Umetufanya nini kwa kututoa Misri? Je, hatukusema huko Misri, 'Tuache peke yetu; tuitumikie Wamisri '? Ingekuwa afadhali kuwatumikia Wamisri kuliko kufa jangwani! "Musa akawajibu ," Msiogope. Simameni imara na mtaona ukombozi Bwana ataleta leo. Wamisri mnaona leo hamutawaona kamwe tena. Bwana atawapigania ninyi; mnahitaji tu kuwa tulivu "(Kutoka 14: 10-14).

Leo tutapata kujua jinsi Waisraeli walijifunza KUSUBIRI MUNGU. Mara tu baadaWamisri kuwaachilia watu hao waende wao wakajuta. Mara moja Farao akaanza kuwafukuza kuwarejesha katika utumwa. Ingekuwa waliona kama ushindi mkubwa wakutoka utumwa ulipotea. Adui aliwafukuza nao wakaogopa mno. Kwa kweli,



### Kupashana Ujumbe

**Ngojea Mungu**

Kila wakati wanafunzi wakisikia "Ngojea Mungu" wakati wa somo, wanafunzi wajibu kwa kusema "Niko tayari" huku wakiruka juu na kufanya ndondi, na kisha kusema "lakini mimi lazima kusubiri" wakiweka mikono yao pamoja na kukaa chini.



www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili

walianza kulalamika na walitaka hata kurudi Misri. Kwa kweli walidhani ingekuwa afadhali utumwa wa kuwa huru badala ya kufukuzwa na adui katika jangwa. Jambo la mwisho walitaka kufanya ni KUSUBIRI MUNGU.

## Uchunguzi wa Angani

### Mungu ni Wakushangaza

Ni ajabu kwamba watu bado walikuwa na hofu hata baada ya kuona utukufu wa Bwana ikiwalinda? Mungu alifanya mambo ya kushangaza zaidi kwa watu hawa walipokuwa wakisafiri! Mungu alimtuma nguzo kikubwa cha wingu ili kuwaongoza wakati wa mchana, na nguzo ya moto mkubwa wa kuwaongoza wakati wa usiku na kuwapa mwanga! Je, unaweza kufikiria zaidi ya watu milioni kutembea katika jangwa na nguzo ya moto mbele yao? Hatujui hasa kiasi cha watu, au urefu wa nguzo ilikuwa, lakini kulikuwa na umati mkubwa, na inaweza kuwa SIO miale ya moto kidogo hio. (Wasomi mahesabu kama kulikuwa na 600,000 \wanaume wa vita, kuna uwezekano hata hadi watu milioni 2 ikiwa ni pamoja na mwanamke, watoto na wanaume wazee.) Hii ni miujiza mkubwa! Mungu aliwaongoza walipokuwa wakisafiri na ishara kubwa isiyo ya kawaida, na hata hivyo bado walikuwa na hofu wakati adui akija kwao.

Wewe na mimi mara nyingi tunapata hofu kama Waisraeli wakati tunajaribu kumtii Mungu. Wakati mwingine mazingira yetu inaonekana kama jangwa bila pa kugeukia huku adui akituandama. Hata baada ya kuona maajabu na ukuu wa Mungu, na miujiza yake, na kukumbuka nyakati ambazo ametuokoa. Lakini wakati tunapata hofu, ni vigumu KUSUBIRI MUNGU.

Israeli pengine walidhani walikuwa na chaguzi mbili, aidha kukimbia au kupigana. Kamwe haikuwa kwa akili yao kukaa tu pale na KUSUBIRI MUNGU. Nani husubiri wakati jambo baya karibu kutokea ??? Kila mtu anajua kwamba lazima apambane au akimbie, lakini Mungu alikuwa na mpango. Musa alisikia mpango wa Mungu na akashiriki na kila mtu ... " Bwana atawapigania ninyi ; mnahitaji tu kutulia . " Mpango wa Mungu ulikuwa ni kupigana vita kwa ajili yao , wakati wao tu ni KUSUBIRI MUNGU!

Ni wangapi wenu wanapenda kukaa na kusubiri? Hakuna mtu! Watu hawa walikuwa katika shida , kama wewe na mimi tunavyo pata shida mara kwa mara. Mpango wa Mungu kwa ajili yao ilikuwa KUSUBIRI MUNGU na basi MUNGU kufanya mapigano. Wakati mwingine unapoingia katika shida , uliza Mungu na uone kama Yeye hataki kufanya mapigano kwa ajili yako. Kazi yako itakuwa sawa kama wana wa Israeli, ni KUSUBIRI MUNGU!

Chumba cha maamkuli

## Nguzo za Wingu

Kituo cha vitafunio

Popcorn inaweza kuwakilisha mawingu, kama lile lililo ongoza Waisraeli katika jangwa.

Kutengeneza nguzo la wingu zamisha fimbo katika syrup ya gamu na kisha ingiza ndani ya bakuli la popcorn ili fimbo iokote popcorn. Waache watoto watengeneze vijiti vyao wenyewe kwa ajili ya kujifurahisha.



Chumba cha maamkuli

## Wazo


Utendaji katika anga kujadiliwa wakati wa kula vitafunio

## Roketi za anga

Tangu mtu aweza kuona mwezi alitamani kusafiri huko. Fikiria juu ya hatua hii ya kushangaza katika safari ya anga: Hivi karibuni baada ya wao "kuondoka" katika njia yao ya mwezi wanaanga watafikia "mbio ya kutoroka" na kuzima injini zao na kuendelea na safari ulio baki. Wakati huo ambao gari umezimwa, roketi inakuwa katika mbio ya haraka sana! Ni sawa wewe na mimi, Mara nyingi, tunafikiri tunahitaji kufanya kazi kwa bidii na kushinikiza kupata kufika tunakotaka kwenda. Hata hivyo, mara nyingi Mungu anatutaka kukaa tu na kusubiri, kama wanaanga wanavyo fanya katika roketi zao. Tuna hitajika tusifanye lolote kabisa, na kuruhusu Mungu atushugulikie. Lazima iwe vigumu kwa wanaanga kuwa katikati ya wasilolijua katika anga kubwa hivyo kisha kuzima injini zao kubwa za roketi ... wakiamini kwamba bado wako kwa mbio ya haraka vile wanavyo hitaji! Tunaweza pia kupumzika tukijua kwamba wakati Mungu anataka tusubiri, Hakika tuko kwa mbio ya kazi!




www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili




Uhandisi





Darasa la Kadeti

## Roketi ya Galaxy Express

Vifaa:
* Nakala ya mfano wa roketi kwa kila mwanafunzi.
* Makasi (Kama wanafunzi watakata roketi zao wenyewe. Watoto wadogo wanahitaji mwalimu kuwakatia roketi zao hivyo wao ni kuunda tu.)
* Crayons au penseli za rangi
* Tape au gamu
Hiari: Tumia bomba tupu la karatasi ya choo.
Hiari: Shikisha nyota au vipande vidogo vya alumini kuongeza urembo.

Maelezo:
1. Kata vipande zote katika mistari yote imara.
2. Paka rangi kila sehemu.
3. Pindua "Galaxy express" iwe bomba kisha funga na mkanda au gamu ili ishikke.
4. Mabawa yakona vidude yakushika chini ya roketi. Elewa zinapitana ili iungane kabla ya kuingia ndani ya mwili wa roketi.
5. Kama unatumia bomba la karatasi ya choo, ingiza na upole kisha pindua na ukunje kwenye sehemu ya mabawa kabla kushikisha na koni huko juu.
6. Tengeneza koni, ukipishana hadi mstari ulio na alama. Funga na mkanda au gamu ishike juu ya roketi.

## Itana kwake Mungu!

Rudia hadithi, Ukifundisha maneno haya katika lugha ya ishara. Kisha peana vitabu vya wanafunzi na kusaidia yeyote aliye na maswali.



### Angalia

Peleka vidole viwili vya kulia mbali na macho.




### Ahadi


kidole cha kulia midomoni; peleka kufungua mkono ngumi upande wa kushoto.

### Watu

Huku gumba na kidole cha katikati ikigusa, tengeneza duara ya ndani na kurudia.



Kurudi hadi kwenye daraja kwa ajili ya michezo na kufunga




## Kugusana juu ya mti

Watoto wawili kushiriki, mmoja kutoka kila timu. Watoto wasimame juu ya kipande cha mbao (2 "na 6"). Lengo ni kuangusha mchezaji mwingine chini kwa kutumia kijiti cha kuogelea kana kwamba ilikuwa ni Upanga , bila kugonga mtu mwingine katika kichwa. Mchezaji anaondolewa mara tu mguu moja unagusa ardhi. Mchezaji aliyebaki lazima asimame tu juu ya mti ili ashinde . Usiweke mbao juu sana, ili watoto wasijidhuru. Badilisha kijiti cha kuogelea na chochote ambacho ni laini isiwe hatari.


## kutengeneza piramidi


Huu ni mchezo rahisi ambapo kila timu inatumia watoto 6 kutengeneza piramidi kwa haraka iwezekanavyo. (Wachezaji watatu kuunda msingi , wakipiga magoti juu ya sakafu , na kutazama watazamaji. Watoto wengine wawili wapige magoti juu ya migongo yao , na mchezaji mdogo zaidi apande juu na kupiga magoti juu ya mstari wa katikati.) Kikosi cha kwanza kukamilisha mafanikio ya piramidi kinashinda!

# 5 Safari ya tano

## Abudu Mungu


Mabandari ya angani:



### Mwanzo wa Nguvu

Mchezo wa kuigiza wa ufunguzi





Leo robot anajifanya kama yeye ndio robot bora zaidi duniani, au hata ulimwengu wa anga, na anataka nahodha kumsifu kwa jinsi alivyo bora. Nahodha anajaribu kusema kuwa Mungu ndiye bora zaidi, si watu, lakini robot ana hakika kwamba yeye ni kamilifu. Robot anasisimka kuwa watakwenda satellite ambaye alitaka kwenda jana, na anasema kuwa kuna cinema kubwa inayo onyesha! Watashuhudia mlipuko wa nyota, supernova! Wao waka jiharakisha tayari kwa ajili ya kuondoka kwenda katika kituo cha anga "Explotelite" ambayo ni satellite.Cheza karibu na kichekesho chako, kuonyesha kwamba robot anadhani yeye anafanya mambo kikamilifu, lakini yeye kwa kweli anafanya makosa. Kwa mfano, wakati wa kendesha meli ya anga, robot anaweza hadaa kwamba anaweza kuruka bila mikono, na kisha kupinduka kufunga kiatu chake. Bila yeye kuona, nahodha ananyakua uendeshaji akwepe kwa shida nyota ya comet ilio kuwa inapaa karibu nao. Baada ya kukosa kuona makosa yake kwa muda, robot anafanya kosa kubwa na kuhisi vibaya.
Nahodha anashiriki neno la siku: "Abudu Mungu," na jinsi inazungumzia juu ya kuabudu MUNGU, sio wewe mwenyewe! Nahodha anafundisha watazamaji na robot kujibu kelele yangu, "nina kuabudu wewe" mikono yao juu, wakipunga hewa. Wanapo karibia satellite, nahodha akatambua kuwa alisahau kutumia ramani za google kwa maelekezo. Yeye hajui jinsi ya kufikia satellite. Baadhi yao wakadhania, baadhi kuomba, waka geuka kulia, kisha kushoto, na mwishowe wakafika kikamilifu katika kituo cha anga! Wote nahodha na robot wakatambua kwamba Mungu ndiye alisaidia wao kupata njia yao na wakapiga kelele pamoja "nina kuabudu" mikono yao juu kwa hewa .
Baada ya kutua, wao wakatoka nje , wakisisimka kushuhudia supernova leo .



### Ujumbe unao ingia . . .

Mstari wa Bibilia

"Msifuni Mungu katika patakatifu pake; Msifuni katika anga la uweza wake." Zaburi 150:1




### Dharula kutoka kwa udhibiti wa Misheni . . .

Somo kuu

Kuvuka bahari ya Shamu

Kisha Bwana akamwambia Musa , "Nyosha mkono wako juu ya bahari ili maji iweza kurudi tena  na kufunika Wamisri na magari yao na farasi . "Musa akanyosha mkono wake juu ya bahari, na alfajiri bahari ikarudi mahali pake. Wamisri wakawa wakikimbia kuelekea huko, na Bwana akawafagia ndani ya baharini. Maji ikafunika magari na wapandao farasi - jeshi lote la Farao walioandama Israeli baharini. Hakuna hata mmoja wao alinusurika. Lakini Waisraeli wakaendelea na safari ndani ya  bahari katika njia kavu , na ukuta wa maji juu kulia na upande wa kushoto yao. Hiyo siku Bwana aliwaokoa Israeli kutoka katika mikono ya Wamisri, na Waisraeli wakawaona Wamisri wamelala wafu katika pwani ya bahari.




### Kupashana Ujumbe

Abudu Mungu

Kila wakati wanafunzi wakisikia "Mwabudu Mungu" wakati wa somo,  wanafunzi wajibu kwa kusema "Ninakuabudu" huku waki inua mikono yao juu katika anga na kukitikisa mbele na nyuma.




www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili



## Uchunguzi wa Angani

### Mungu ni Wakutisha


Ndipo Musa na wana wa Israeli waliimba wimbo huu kwa Bwana;
"Nitamwimbia Bwana, kwa maana ametukuka sana.
Wote farasi na dereva aliwatupa baharini.
Bwana ni nguvu yangu na mtetezi wangu; Amekuwa wokovu wangu.
Yeye ni Mungu wangu, nami nitamsifu, Mungu wa baba yangu, nami nitamtukuza" (Kutoka 14: 26-30, 15: 1-2). Wakati tuliacha Israeli jana; walikuwa katika shida na kukabiliwa na maadui wao ambao walikuwa wakiwafukuza. Walitaka kupambana au kukimbia, lakini waliamua KUSUBIRI MUNGU. Walijikuta wamenaswa kati ya jeshi la adui na bahari kubwa "Bahari ya Shamu." Walikuwa wamenaswa na kusubiri Mungu aje kuwaokoa, na Mungu AKAFANYA HIVYO! Hebu tumwabudu Mungu!
Mungu alimwagiza Musa kushikilia fimbo yake juu ya bahari na mara maji ikaanza kujigawa mara mbili! Bahari kubwa nzima ukagawanyika na kuwapa njia nzuri kavu kutembea kuvukia nchi kavu! Huu ni moja wa miujiza ya kushangaza zaidi katika Biblia. Bahari kusimamishwa na kuinuka ili zaidi ya watu milioni kutembea kuvuka. Kisha Wamisri walipojaribu kuwafuata, Mungu akaruhusu bahari kurudi na kuwamaliza, na kuwaua wote! Huu ni mfano wa Mungu kuwapigania vita kwa ajili yenu! Hakuna lingine la kufanya ila KUMUABUDU MUNGU kwa miujiza yake ya ajabu. Je, unaweza kufikiria kuvuka bahari katika nchi kavu na kuona Mungu akishinda adui zenu, mbele ya macho yenu?
Jambo la kwanza walivyofanya ni kuimba nyimbo za sifa kwa Mungu, kumwabudu kwa ajabu na ushujaa wake.
Hio lazima iwe jibu letu la kwanza kwa Mungu na maajabu zake pia, KUMUABUDU MUNGU! Unapo uliza Mungu akusaidie na mtihani katika shule , na yeye anafanya hivyo , si kukaa tu pale . Umshukuru! Wakati unajisikia vizuri kwa kufanya vyema kwenye mtihani huo , MUABUDU MUNGU! Wakati wewe umechoka kuona wazazi wako wakipigana na kuomba kwa Mungu awape amani , na wao ghafla wakaacha vita, MUABUDU MUNGU! Baada ya kuuliza Mungu akuone na akupe mradi wa kusaidia katika kanisa, na mwalimu wa darasa anakuuliza wewe kuwa msaidizi wao, MUABUDU MUNGU. Baada ya kuuliza Mungu kukusaidia kuepuka au kusimama na mchokozi shuleni, na mchokozi na familia yake nzima kupata kuhamishwa mji mwingine, MUABUDU MUNGU! Siku zote kutakuwa na majibu tofauti kutoka kwa Mungu kwa aina ya matatizo tunayokabiliana nazo . Mungu kila wakati anatusaidia na inatubidi sisi kujibu kama walivyofanya Israeli : KUMUABUDU MUNGU!



Chumba cha maamkuli

## Kuvuka Bahari katika Ardhi Kavu

Kituo cha vitafunio




Tengeneza gelatin ya bluu, na kumwaga katika bakuli kubwa kuunda. Kama inahitajika, weka peremende wenye umbo wa samaki ukiwa na gamu katika Jello kabla kuundika kabisa. Ondoa sehemu ya katikati kuwakilisha nchi kavu ambaye wana wa Israeli walitembelea katika bahari ya shamu. Tengeneza moja kwa ajili ya kuonyesha, lakini andaa vikombe ndogo za Jello kwa kila mtoto ya kukunywa nayo.






**Wazo** Utendaji katika anga kujadiliwa wakati wa kula vitafunio

## Supernovas

Baadhi za nyota ziko kubwa na kuwa na shinikizo la upepo mkubwa ndani yao na inafika sehemu ambayo hawawezi kustahimili shinikizo tena. Zina fura na kufura na kufura mpaka nyota ZINALIPUKA kuwa milioni ya vipande vidogo katika anga! Wanasayansi wanaita hivi vipande supernovas. Siku hiyo Israeli waliokolewa kutoka utumwa na kifo kupitia kuvuka bahari ya shamu, shukrani na furaha lazima ikawa shinikizo kubwa ndani yao. Naweza fikiria ilibidi walipuke kwa shukrani na kumwabudu Mungu wao ambaye aliye waokowa! Kama vile supernova, wewe na mimi pia tuna wakati Mungu anakuja kutuokoa na hatuna lingine ila kulipuka kwenye ibada; tukishukuru Mungu kwa kutuokoa!








## Darasa la Kadeti

### Itana kwake Mungu!

Rudia hadithi, Ukifundisha maneno haya katika lugha ya ishara. Kisha peana vitabu vya wanafunzi na kusaidia yeyote aliye na maswali.

**Imba**

Peleka mkono wa kulia mbele na nyuma mbele ya kiganja ya kushoto





**Ishi**

Vidole gumba na ya kati kupanuliwa, peleka mikono juu ya mwili.



**Sherehekea**


Kidole gumba na kati zikigusana, fanya duaru ndogo ndogo

## Uhandisi

### Kuvuka Bahari ya Shamu

Vifaa:
Karatasi nyeupe uliochapishwa aya au nakala ulio na bahari. Crayons za buluu, penseli za rangi, za alama, au rangi.
Maelezo:
1. Paka rangi sehemu ya maji na nchi kavu.
2. Kata au pasua kwenye mashimo ya mistari, simama kabla ya kufikia sehemu ya nchi kavu.
3. Zungusha vipande kwenye fimbo na ukase, penseli, au crayon. Ni hiari: paka Gundi mawe kidogo yenye ndani ya bahari.

## Kurudi hadi kwenye daraja kwa ajili ya michezo na kufunga





### Kuangusha Marshmallow


Wazo la mchezo huu ni kuwa na timu kushindana kuona ni jinsi gani marshmallows nyingi inaweza wekawa katika kikombe kutoka paji la uso la mwenzao wa timu yao. Inafurahisha kufanya mchezo huu wa ziada kwa ajili ya watazamaji kufurahia.
Weka ngazi au kiti mbele na watoto wawili kushikilia iwe imara. Kila timu inahitaji watoto 5 kushiriki, na timu moja tu inakwenda kwa wakati mmoja, ikilindwa kwa makini na mlinzi!
Watoto wawili (au watu wazima viongozi) watalala chini mbele ya ngazi kichwa-kwa-kichwa. Kulinda nguo za watoto chukuwa mifuko za takataka kisha kata shimo kuingiza kichwa, na kuvaa kama shati. Pia ingekuwa vizuri watoto hawa wawili kuvaa miwani ya kinga. Weka marshmallows na syrup ya chocolate kwa viwango sawa katika bakuli mbili.
Mtoto mmoja anaenda juu ya ngazi na bakuli ya marshmallows. Watoto wawili kushikilia ngazi na watoto wawili kulala juu ya ardhi, wameshikiliaa kikombe kwenye paji la uso. Wakati kiongozi anasema 'Nenda', mtoto aliye juu ya ngazi anajaribu kuangusha marshmallows ilio na chocolate katika vikombe kwa haraka kwenye sekunde 60. Mwishowe, hesabu marshmallows katika kikombe. Marshmallows ilio liwa usi hesabu! Baada ya timu moja kumaliza, anzisha timu ya pili. Timu yenye marshmallows zaidi inashinda!

### Relay ya Keki


Wazo la mchezo huu ni kupata watoto wawili kutoka kila timu kupamba keki kwa haraka iwezekanavyo kama relay, inafurahisha kuangalia na kwa watazamaji kwa ujumla. Tayarisha kabla ya muda mikate miwili ambayo haina barafu. Chukua aprons, barafu, visu na vitu vya kunyunyuzia au njia nyingine ya kupamba keki kidogo. Wakati kiongozi anasema anza, watoto wanavaa aprons, wanatia keki barafu, nakupamba, na kuuma keki na mdomo. Timu ya haraka sana ni mshindi. Kama ziada, toa keki ya kutosha kufurahisha peana kwa watoto wote mwishoni mwa VBS yako!


Kwa sauti yangu
namwita BWANA
Zaburi 3:4



Kwa sauti yangu
namwita BWANA
Zaburi 3:4




“Mimi hapa, nitume mimi!”
Isaya 6:8





“Mimi hapa, nitume mimi!”
Isaya 6:8



"Msifuni Mungu
katika patakatifu
pake;
Msifuni
katika anga
la uweza
wake."
Zaburi 150:1







Galaxy Express
Galaxy Express

# Habari Watoto

Mumealikwa kupanda ndege ya angani...




Ni safari ya anga, ambayo mutagundua ukuu wa Mungu! Kutakua na vinywaji tamu, ufundi, shughuli, nyimbo, roketi  na vitu vingi vya kufurahisha. Njoo ujiunge nasi!




**Wapi:**

**Lini:**

# Habari Watoto

Mumealikwa kupanda ndege ya angani...




Ni safari ya anga, ambayo mutagundua ukuu wa Mungu! Kutakua na vinywaji tamu, ufundi, shughuli, nyimbo, roketi na vitu vingi vya kufurahisha. Njoo ujiunge nasi!

**Wapi:**

**Lini:**

---



# Ime tuzwa kwake:


[ _______________________________________ ]

Kwa ajili yakushiriki kwenye shule ya bibilia ya likizo “Galaxy express”

Imepeanwa na: _______________________________

# Mtandao,haraka

***Toa kwenye tovuti ratiba ya VBS na shule la jumapili ikiwa mzima bure.***



- **vitabu vya mwalimu**
- **vitabu vya mwanafunzi**
- **muziki**
- **video**
- **kijitabu cha kituo(VBS)**
- **mabango**
- **peperushi  la mwaliko**
- **Cheti**
- **usuli wa jukwaa**

Zote zinapatikana kwenye mtandao unaweza zitoa hapo.(downloads)
Pia tafuta maelezo vile utatumia hii programu na mawazo ya kufanya programu yako ya kufana!

**Nyenzo yetu ni bure kutoa kwenye mtandao,bure kutumia, bure kupiga chapa na bure kusambaza kwa makanisa mengine na huduma bila majukumu**




**Toa kwenye tovuti (download)program mzima BURE!**

**www.ChildrenAreImportant.com**

**Watoto ni wa muhimu**






## Rahisi
Wenye umri toka 4-6,hakuna kusoma

## Wastani
Wenye umri wa 7-9,baadhi ya kusoma

## Ngumu
Wenye miaka 10-12,kusoma na mafumbo magumu




## Vitabu vya mwanafunzi
Wanafunzi kwenye VBS yetu watafurahia kufanya mafumbo na shughuli huku wakipitia somo la kila siku

Ili Kuipa timu yako mipango kamili na kufanya VBS kuwa bora katika safari yako ya anga i! Vifaa vyote katika kurasa huu yana chapishwa kwenye mtandao na zinapatikana bure . Pia pata nembo na graphics kwenye mtandao ili kujitengenezea vifaa vyako mwenyewe. Wape walimu wako msisimko na kusaidia watoto wako wapate vifaa vingi vya kufurahisha kujifunza juu ya Yesu!

Watoto ni wa muhimu

# www.ChildrenAreImportant.com/galaxy

*Ukitaka kupewa hitaji kubwa (ya makanisa 100+) wasiliana nasi na unukuu vifaa vya kingereza au kihindi.*
*Tuko Mexico: 01-592-924-9041*
*info@ChildrenAreImportant.com*

## Vijitabu vya kiongozi
Kwa urahisi,maelezo maalum kwa kila idara ya VBS imewekwa ndani ya vijitabu tofauti kupatia viongozi.maelezo haya yanapatikana pia kwenye kijitabu cha mkurugenzi.

## Mwongozo wa mkurugenzi
Pata maelezo yote ya "Galaxy express" VBS kwenye kitabu hiki kimoja-ratiba,masomo,na mawazo Zaidi










## Bango la sayari lishaa wekwa

Kwenye siku ya pili ya VBS,tumia vibango kuonyesha ukubwa wa sayari na nyota kwenye anga  letu.




## Bango la kualika

Angika bango hili kwenye majirani wanaowazunguka kualika watoto Zaidi kwenye tukio lako







## CD na DVD za muziki

Fanya VBS yako ikue na furaha Zaidi kwa kutumia muziki na densi zetu za kiasili ikiwa imeundwa kwa "Galaxy express" VBS! toa muziki kwenye mtandao na uone video kwenye Youtube.(muziki iko kwa kiingereza tu mara hii)




## Kipeperushi cha maaliko

Ambia watoto Zaidi kuhusu yesu kwa kuwaalika kwenye tukio lako na vipeperushi hivi




## Cheti

Wape watoto zawadi ya cheti hiki kwa kuhudhuria tukio lako

## Ufundi


Watoto wanapenda ufundi "Galaxy express" inakuja na seti ya hila,moja kila siku,ikiwa na mifumo.tumia vifaa ambazo zinapatikana ndani ya nchi ili kusaidia watoto kuwa na raha wakiongeza nguvu masomo yao ya kila siku. kila hila imeundwa kutumia kipande kimoja cha karatasi kwa mtoto mmoja,pamoja na gundi na vifaa vya kupiga rangi.






## Nyuma ya jukwaa(background)

Hamasisha fikra za watoto na nyuma ya jukwaa kwa ajili ya jukwaa lako.toa kwenye mtandao PDF na agizo  la tarp iliyo pigwa chapa.kipimo kilicho pendekezwa: 4x2m or 3x1.5m





www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili

Manual Galaxy Swahili

13602

www.ChildrenAreImportant.com
info@childrenareimportant.com
Tunapatikana Mexico.
DK Editorial Pro-Visión A.C.

Watoto ni wa muhimu